



# Kuishi Maisha Yenye Afya



## Kwenye Kingo za Mto Tana

Healthy Living Beside the River Tana




This manual was designed by the Community Health Division  
**KENYA WATER FOR HEALTH ORGANISATION (KWAHO)**  
for the Lower Tana River Shallow Well Programme.

Developed and illustrated by Juliet Waterkeyn.

# Kuishi Maisha Yenye Afya Kwenye Kingo za Mto Tana

THE TANA RIVER DISTRICT WATER SUPPLY  
DEPARTMENT  
P.O. BOX 203, NAIROBI  
TEL: (070) 814311 ext. 141/142  
ISSN 7100  
DOI 203.289kl

Healthy Living Beside the River Tana



Kifaa cha kufundishia kilicho tengezewa wafanya kazi wa afya katika wilaya ya Tana River kwa ugawaji miongoni mwa vikundi vya wanawake vya Orma na Wadei na mabaraza ya maji katika maeneo ambayo tayari yamepata maji safi.

A teaching aid developed for health workers in the Tana River District for distribution amongst the Orma and Wadei Womens' Groups and Water Committees in areas where protected water has already been obtained.

# Chairman's Foreword

KWAHO has embarked on many serious programmes to accelerate community training in water and sanitation in support of government overall objectives of achieving health for all Kenyans by the year 2000.

The provision of safe drinking water is one of the most fundamental requirements in the project areas where KWAHO operates. However, it is important that water provision is coupled with the full understanding by the communities of the connection between personal hygiene and methods of water utilization with many water-related diseases. This is also one of the key elements of Primary Health Care which is being addressed in Kenya, in the Child Survival and Development Programme.

Although KWAHO has an extensive network of "water for health assistants" working in the field, providing the training that is so vital a component in any community-based project, these field officers have little in the way of teaching aids to make their message clear. This booklet was therefore developed as part of a series that aims to provide a manual for each project area, dealing specifically with the technologies used in the area and relating to the particular health problems of the district.

Three such booklets have been produced to date, relating to water supply projects in Kwale District (in Swahili), South Nyanza District (in Luo) and this particular one (in Swahili), which reflects the problems of those communities living on the banks of the Tana River, in the District of that name in Coast Province. The illustrations are intended to provoke discussion and convey specific messages on health matters related to each particular community, and for this reason, the booklets should be used only in the areas for which they were designed.

It is a pleasure to note that KWAHO in its small way is contributing towards the remedy of these problems by developing a training system that should create a more general awareness among the communities living in the project areas.

This booklet is intended to supplement what the Ministry of Health is striving to achieve in these areas and this effort is highly appreciated. It is therefore my sincere hope that this booklet will be made use of in the way that it deserves and that it will go a long way towards ensuring that the training activities in KWAHO's project areas achieve the desired goal of improving community health through the knowledge and practice of better hygiene in the home.



James A. Aremo

*Chairman, KWAHO*

# Executive Summary


Kenya Water for Health Organization (KWAHO) is an indigenous Non-Governmental Organization which supports community efforts in the rural areas to achieve safe drinking water and better sanitation facilities.

To achieve sustainable projects, KWAHO places great emphasis on community mobilization at every stage of the project. To this end, methodologies have been developed whereby rural communities are involved from the beginning, with project identification and planning, and follow through with the implementation of the project. KWAHO's role is to train community leaders and village technicians in operation and maintenance, so ensuring an ongoing water supply. The training of men and women at the village level has, therefore been one of KWAHO's major concerns.

Whilst the primary goal is to supply clean water, this benefit to health can be lost through poor hygiene practices due mainly to ignorance of health hazards. With effective training, these habits can be changed without undue demands on the workload of the women themselves, or on their income, so ensuring a more healthy life for communities where clean water is already available.

For this reason, KWAHO has set up a division of Community Health, with a section producing health education material suitable for the project areas concerned. Although to date these messages have focused on the much needed subject of water-related diseases and sanitation, there are many other concerns besides these that are crucial and need to be addressed if a healthy family is our objective. With the formation of a Women in Development Division within KWAHO, there is the need to focus on a more broadly based type of training material, which should encompass nutrition, immunization and home industries.

This booklet therefore, developed for the Orma and Waday communities living at Wema and Garsen, Tana River District, is intended as the basic training manual in water-related diseases, for KWAHO's Shallow Well Programme, where by the end of the first phase (1989) over 40 wells had been supplied. In line with KWAHO's 'culture specific' approach, a separate training material has been developed for the Pokomo communities living in the area. As KWAHO has water projects in every province throughout the country it is expected that eventually each area will be catered for, until a comprehensive series of training material exists. In this way, KWAHO hopes that this will also help to compliment government programmes in these areas.



Margaret Mwangola

*Executive Director, KWAHO*

## Contents

Chapter	
1. Viini Ni Nini? .....	3
<i>What is a Germ?</i>	
2. Viini Vinatawanyika Namna Gani? .....	10
<i>How are Germs Spread?</i>	
3. Viini Vinaweza Kutufanyia Nini? .....	16
<i>What can Germs do to us?</i>	
4. Jinsi ya Kukinga Jamaa Yako kutokana na viini.....	25
<i>How to Protect your Family from Germs</i>	
5. Kichocho.....	30
<i>Bilharzia</i>	
6. Magonjwa yanayohusika na Maji .....	38
<i>Other Water Related Diseases</i>	
7. Kamati za maji .....	43
<i>Water Committees</i>	
8. English Key .....	45

This manual was designed by the Community Health Division  
**KENYA WATER FOR HEALTH ORGANISATION (KWAHO)**  
for the Lower Tana River Shallow Well Programme.

Developed and illustrated by Juliet Waterkeyn.  
Health messages developed by Wilson Kinoti and Sr. Agnes Reinkemeyer.  
Pretested with the help of the Orma and Wadei Communities.  
Translated by Suleiman Juma, assisted by Connie Kiprop.  
Funded by WaterAid 1989.

---

Published by the Kenya Water for Health Organisation (KWAHO), P.O. Box 61470, Nairobi,  
Tel: 556068, 557550, 557088

Printed by the African Medical and Research Foundation (AMREF), Wilson Airport  
P.O. Box 30125. Nairobi

# VIINI NI NINI?

## Unajua viini ni nini?

Viini ni vijidudu vidogo sana ambavyo hatuwezi kuviona kwa macho matupu. Ingawa hatuwezi kuviona viko kila mahali. Hivi vijidudu vina manufaa kwetu. Bakteria kwa mfano zinatumiwa kwa kutengeneza dawa za kuponya watu - penicillian na aina ya kovu inayoua viini vingine.

## Maziwa huganda namna gani?

### Na pombe huchacha vipi?

Kuna vijidudu (Bakteria) ndani ya vyakula vyote.

Hiyo ndiyo sababu chakula huharibika na kuoza.


Kwa upande wamaziwa au pombe tukitaka maziwa yagande au pombe ichache tunaviacha vijiduduhivi vi fanye kazi yao kwa sababu vijidudu vyenyewe vina manufaa kwetu. Ingawa hatuvioni lakini viko na vinatufanyia kazi. Unaweza kuviona kwa darubini.

Hata hivyo, sio vijidudu vyote vina manufaa. Vijidudu vingine vinaleta magonjwa na vingine vinaharibu damu na ngozi zetu.



# Tunatumiaje maji ya mto?







# Kunywa maji ya mto

**Je, haya maji ni salama kunywa?**

La, haya maji ni hatari kwa sababu yamechafuliwa na wanyama na kinyesi cha wanadamu.

**Kitu gani kitatokea ikiwa utakunywa maji haya?**

- Utapata
1. Kichocho
  2. Kuhara
  3. Kutapika
  4. Michango

**Je, kuhara huletwa namna gani?**

Bi. Fatouma hakujua jinsi kuhara kunavyoletwa. Hapa anateka maji ya kunywa mtoni. Haya maji yanaonekana masafi kwa hivyo, anayanywa. Hawezi kuamini kwamba kuna kitu cho chote kibaya mpaka akione. Lakini kuna vitu vingine vidogo sana ambavyo hatuwezi kuviona kwa macho yetu. Wataalamu wakituambia tukubaliane nao.




# Uchunguzi ma maji kwa Durubini

**Viini ni nini?**

**Unaweza je kuviona viini?**

Daktari akiyaangalia maji haya ambayo Bibi Fatouma ameyanywa kwa darubini hivi ndivyo anavyoona. Haya maji yana vijidudu vinavyoogelea na vinaishi humu. Hivi vijidudu vinaweza kuwa na manufaa na madhara kwa mwanadamu. Vijidudu vinavyoleta madhara vinaitwa viini na vinaweza kufanya madhara kwa miili yetu kwa kuleta ugonjwa kwa miili yetu.



# Maji ya mto yana vijidudu mpaka uyachemshe

## Njia zingine za kutakasa maji.

1. Kwa kuyachuja kabla ya kunywa.
2. Kwa kuruhusu maji yasimame mpaka uchafu utue chini (mitungi mitatu). Kichocho ndani ya maji kitakufa kama maji yatahifadhiwa kwa siku mbili (Masaa 48).
3. Tia dawa aina ya Aluminium Sulphate ambayo inafanya matope kuganda na kutua chini.
4. Watu wengine wanatumia Jik.



## Je njia hizi hutakasa maji kabisa?

Njia hizi zinasaidia na tusiziache lakini sio salama sana kwani viini bado vina baki ndani ya maji na baadaye vinalete magonjwa.

## Kwa nini kuchemsha maji ni njia ya pekee iliyo salama ya pekee ya kuua viini?

Kwa sababu ioto jingi huua viini. Kuhakikisha kuwa vijidudu vyote vimekufa lazima uyachemshe maji kwa dakika sita zaidi baada ya kuchemka.

# Maji masafi— Mtambo wa mkono



## Maji masafi hupatikana wapi?

1. Kutoka kwa mitambo ya mkono.
2. Kutoka kwa chemchemi.
3. Maji ya mvua kutoka kwa paa za nyumba.

## Je, kuna haja ya kuchemsha au kutakasa maji haya?

La, haya maji ni safi kabisa.

## Kwa nini unadhani maji yanayotoka ardhini ni safi?

Kwa sababu maji yanayotoka ardhini hayawezi kuchafuliwa na kinyesi cha au wanyama. Haya maji yanaweza kuchachafuliwa tu ikiwa kuna choo kisiichozi mita 30 kutoa mahali hapo Kinyesi kinaweza kupenya kisimani na kuyachafua maji. Hata hivyo, ikiwa choo ni zaidi ya mita 30 haya maji yatachujwa na yatakuwa safi.

## VIINI VINAENEZWA NAMNA GANI?

### Mikono yetu hutawanya viini

Abdi ametoka kwenye zizi ambapo alikuwa anaondoa samadi ili achome. Kuchoma samadi kila siku ni mazoza mazuri. Inahifadhi usafi na hupunguza inzi.



### Viini vinapanda namna gani kwa mikono yetu?

Tunapofanya kazi, tunagusa vitu vingi ambavyo ni vichafu.

### Ni vitu vya aina gani vinavyo fanya mikono yetu kuwa michafu?

1. Kukama ng'ombe au kugusa wanyama.
2. Kukusanya samadi ya ng'ombe kwa mikono.

### Uchomaji wa samadi hupunguza nzi kwa njia gani?

Kwa sababu inzi wanavutiwa na samadi wanataga mayai juu yake. Moto utaharibu mayai hayo.

### Je, moto una kazi gani zaidi?

Ni mpango mzuri kuchoma takataka, chakula kilichooza, mifupa na kadhalika kila siku. Ikiwa takataka zitaachwa karibu na nyumba zitawavutia inzi nyumbani kwetu. Inzi wataleta viini utoka kwa samadi na kuchafua chakula chetu.

## **Kutayarisha chakula kwa mikono michafu husababisha kuhara**



**Inzi hubebaje viini**

**Inzi pia hubeba viini**

Inzi wanavutiwa na vitu vichafu ili wapate chakula na watage mayai hapo. Wanaenda kwa kinyesi cha wanadamu na wanyama na aina zote za nyama na mboga zilizoza, vidonda na chakula chetu.

**Inzi wanatawanya viini namna gani?**

Viini ni vidogo sana hatuwezi kuviona kwa macho matupu. Inzi wanatembea juu ya vitu vichafu halafu wanaingia jikoni.

Wanapotembea juu ya chakula chetu tayari miguu yao ni michafu na inabeba viini vinavyosalia juu ya chakula chetu. Hapo ndipo tunakula viini hivi ndani ya chakula chetu.

Viini viko kila mahali hasa katika kinyesi cha wanadamu au wanyama. Viini vinaingia ndani ya milli yetu kupitia majeraha, mdomo, pua, macho, masikio na mahali pa haja ndogo. Viini viko kila mahali hasa katika kinyesi cha wanadamu au wanyama.

# Uchafuzi wa chakula na maji yakihifadhiwa vibaya

Ingawa Bi. Fatouma anayachota maji masafi kutoka kwa mtambo wa maji jamaa zake wangali wanaugua ugonjwa wa kuhara.



**Unaweza kutona kinachosababisha shida zake katika picha hii?**

1. Abdi amekuwa akicheza kwenye uchafu hapo nje. Ana kiu na amekuja kunywa maji. Mikono yake ni michafu lakini amekibeba kikombe na kutumbukiza mikono ndani ya maji. Mikono yake imeacha viini ndani ya maji. Sasa jamaa wote wataugua ugonjwa kuhara kwa sababu ya mikono michafu ya Abdi.

2. Mbuzi na kuku wanaruhusiwa kuingia ndani ya nyumba na hali vyakula vimeachwa bila kufunikwa na vyombo vyote vimeachwa sakafuni. Mbuzi wanalamba masahani na hali walikuwa wanakula takataka hapo nje. Mdomo yao ni michafu.
3. Kuku wanakanyaga chombo kilicho na maji ya kunywa. Hicho chombo hakina kifuniko kwa hivyo, kinyesi cha kuku kinaingia ndani ya haya maji na kuyachafua.
4. Inzi wanatua juu ya vyombo ambavyo vimeachwa ovyo kila mahali. Inzi wanatembea juu ya chakula na kuacha viini. Lakini kuhara kunaweza kuzuiliwa kwa kufunika chakula na maji.

### **Unajua magonjwa mengine yanayoua na yanaletwa na kunywa maji machafu?**

1. Kipindupindu—homa, kuhara sana, kumalizika kwa maji mwilini, unyonge na kifo.
2. Ugonjwa wa ini—maumivu tumboni, homa, macho yanakuwa manjano na kuwa mnonge.
3. Homa ya tumbo—kuumwa na kichwa, homa, maumivu ya tumbo, kuhara na wa.siwasi.
4. Kuhara damu—kuhara sana, kumalizika maji mwilini na homa.

Viini viko kila pahali hasa katika kinyesi cha wanyama au binadamu. Viini vinaweza kuingia ndani ya miili yetu kupitia majeraha, mdomo, pua, macho, masikio na mahali pa haja ndogo.

### **Viini vinaingiaje ndani ya miili yetu kupitia mdomo?**

Mikono yetu inabeba viini na kuingiza ndani ya miili yetu. Tunaweka mikono mdomoni tunapokula. Kwa hivyo, chakula na maji ni njia muhimu ambazo viini vinatumia kwa kuingia ndani ya miili yetu.



# Kunawa mikono bila sabuni hakuondoi viini vyote

## Jinsi ya kukuza tabia hii?

1. Kama wangetumia sabuni wangukuwa na mikono safi. Sabuni huondoa jasho na mafuta mikononi. Maji huondoa vumbi tu. Sabuni huondoa viini vinavyojificha chini ya makucha.
2. Jamaa wote wanatumia taulo moja. Ikiwa mmoja wao ana ugonjwa ya ngozi basi wote wataambukizwa. Ni bora kuwacha kutumia taulo ili mikono ikauke yenyewe
3. Watu wote wasitumie maji yale tu kwa kunawa mikono. Njia bora zaidi ni kila mtu amwagiliwe maji kutoka chombo kingine.



# Kula chakula kichafu kunaweza kulete kuhara

## Chakula hiki kimechafuliwa namna gani?

1. Mbuzi wamelamba masahani.
2. Chakula kimetayarishwa kwa mikono michafu.
3. Chakula kimekuwa baridi.
4. Inzi wanatembea juu ya chakula na kutawanya viini.
5. Wanakula kwa mikono ambayo hawakunawa vizuri.

## Tunaweza kufanya nini ili kuzuia uchafu huo?

1. Tumia chakula chote baada ya kupika.
2. Hifadhi chakula kilichosalia kwa kufunika vizuri.
3. Usiruhusu mifugo kuingia ndani ya nyumba.
4. Nawa mikono kwa sabuni kabla ya kushika chakula.



# VIINI VINAWEZA KUTUFANYA NINI?



Je, jambo hili linaendelea kwa jamaa yako?

## **Kuhara na kutapika husababishwa na chakula kibaya au maji machafu.**

Mohammed anajisikia vibaya. Anasikia tumbo limejaa na anataka kutapika.

Abdi ameanza kutapika. Wakati mwingine ugonjwa ukizidi mtu atasikia kutapika na kuhara kwa wakati mmoja.

Ali anahara sana. Hawezi kujizuia na tumbo lake limevimba. Anaendelea kuhara wakati wote na amekuwa mnyonge.

### **UNAWEZA KUFANYA NINI ILI KUEPUKA KUHARA NA KUTAPIKA**

1. Nawa mikono yako kabla ya kutayarisha chakula. Kila mara tumia sabuni.
2. Nawa mikono yako baada ya kujisaidia au baada ya kumuosho mtoto akijisaidia.
3. Usile chakula kilichoachwa ovyo tu, kwa vile kitakuwa kimeharibika au kimechafuliwa na inzi.
4. Kula chakula moto.
5. Usimruhusu inzi jikoni.
6. Usiwaruhusu kuku na mbuzi jikoni.
7. Weka kiwanja chako katika hali ya usafi kwa kuchoma takataka zote na pia choma samadi ya n'gombe.
8. Osha vyombo vyote pindi baada ya kula na uvikaushe kwenye mahali pa kukausha vyombo lakini sio sakafuni.
9. Kila mara osha matunda na vyakula vingine vinavyoliwa vbichi kabla ya kuvila.
10. Siku zote osha matunda na chakula choteambach ni kibichi kabla ya kukila.

# Ukosefu wa maji mwilini kutokana na kuhara unaweza kuwaua watoto



Ali amepoteza maji mengi mwilini kwa sababu ya kuhara na anasikia kiu na ni mnyonge.

Huu ukosefu wa maji unaweza kuua watoto kama wataachwa bila maji kwa muda mrefu.



# **Kama mtoto hatapata nafuu baada ya siku moja mpeleke kliniki [zahanati]**

Ali amekuwa akihara kwa siku tatu sasa. Bi. Fatouma anagundua kuwa hali ya Ali itakuwa mbaya kama hampelika hospitalini. Muuguzi ana wasiwasi anapona jinsi Ali amekuwa mgonjwa na anamueleza Bi. Fatouma kuwa angemleta mtoto mapema.


Muuguzi anaeleza kuwa kuna aina mbili za kuhara. Moja ni ile inayoweza kuponywa nyumbani kwa kunywa maji na kula chakula kizuri. Aina ya pili ni ile ambayo inahitaji dawa za kuua viini na hizi dawa zinapatikana kwenye zahanati (kliniki). Kama kuhara hakuapona basi ni kule kuhara hatari zaidi.

**Ali alikuwa karibu kufa**



## **Dalili za ukosefu wa maji mwilini ni zipi?**

1. Mdomo hukauka na kupasuka.
2. Macho yanadidimia.
3. Hakuna machozi mtu anapolia.
4. Mkojo huwa kidogo na ina harufu mbaya.
5. Ngozi hukauka sana.
6. Kwa watoto wadogo utosi hudidimia.



## **Unaweza kukumbuka wakati mwingine ambapo mwili huwa na ukosefu wa maji?**

1. Wakati wa joto jingi na tunapotoa jasho jingi na hali hatuna kitu cha kunywa.
2. Tunapokuwa na homa mwili huwa na joto jingi kwa hivyo, mwili hupoteza maji mengi.

Wakati mwili unaonekana hauna maji lazima mgonjwa apate maji mengi kiasi anachoweza. Kama akitapika, mpe kidogo kidogo kwa kijiko baada ya kila dakika chache. Hiyo ndiyo njia nzuri na rahisi kwa mama kutumia ili kumsaidia mtoto mgonjwa ambaye hana maji mwilini na anahara.

# Kila mara mpe mwenye kuhara maji mengi ili kuzuia maji kumalizika mwilini

**Utafanya nini kama mtu anahara au ana ukosefu wa maji mwilini?**

1. Endelea kumpa kinywaji kila wanapotaka hasa baada ya kuhara.
2. Kama watoto hawajiwezi kabisa uwape maji kidogo kidogo kwa kijiko. Mtoto anahitaji vikombe vitano vya kinywaji kila siku na mtu mzima ana hitaji lita mbili kila siku ili kuzuia ukosefu wa maji mwilini.



## **Vinywaji gani ni bora kwa mgonjwa?**

ORS za paketi, maji ya matunda hata soda ambayo itawapa moyo wa kunywa kitu. Maji yo yote safi hata kama ni chai, maji ya sukari au asali, au maji ya mchele. Supu ni bora zaidi kwani itawapa nguvu.

Ali alipewa maji maalum ya inayoitwa Oral Rehydration Solution (ORS) inayonunuliwa dukani na inachanganywa na maji. Hicho kinywaji hurudisha chumvi na maji yaliyopotezwa mwilini na hufanya mwili kuwa na nguvu tena.

Hiki kinywaji kinaweza kutengenezwa nyumbani kwa kuweka chumvi kidogo, sukari mkono mmoja na maji yaliyochemshwa kikombe kimoja. Hata hivyo, tengeneza kinywaji hicho kwa mashauri ya wauguzi ama sivyo, mchanganyiko huo inaweza kuwa na madhara zaidi.



## Kutompatia mtoto chakula anapohara kunafanya hali yake kuwa mbaya zaidi

Bi. Fatouma anahakika kuwa akimpa Ali chakula wakati anapohara kitamfanya kuwa mgonjwa zaidi. Maskini Ali hajala cho chote na matokeo yake ni kuwa baada ya siku mbili amechoka na dhaifu.



## Utasikiaje ikiwa hutakula kwa siku moja au mbili?


Itakuwaje kwa yule ambaye anahara na kutapika ikiwa hatapata chakula kwa siku moja au mbili?

Baada ya kwenda kliniki alijna jinsi ilivyo muhimu kuendelea kumpqa mtoto mgonjwa chakula kwa kiasi kidogo ili kuendelea kumpa nguvu.



Wagonjwa wanahitaji kula ili wapate nguvu ili mwili uweze kupigana na viini vya magonjwa. Ingawa hawezi kutaka kula, ni sharti apewe chakula nyororo kidogo kidogo kila mara. Mtoto asiyepata chakula cha kutosha anaweza kufa kwa kuhara kwa sababu ya njaa. Mtoto mwenye nguvu anaweza kupigana na kuhara kuliko mtoto mnyonge na ambaye hapati chakula kizuri. Bi. Fatouma anajua chakula kilichopikwa vizuri na nyororo kitasaidia mtoto kupona haraka.

# Sikuzote mpe mtu ambaye anahara chakula kingi ili kuzuia ukosefu wa maji mwilini



**Jeni sawa kumpa mtoto kupewa chakula hata kama anahara punde tu baada ya kula?**

Ndiyo. Ni muhimu kujaribu kumpatia mtoto chakula. Hata kama ikionekana chakula hakibaki tumboni lakini kuna kiasi kidogo kinabaki.

**Chakula cha aina gani kinafaa kwa mtoto anayehara?**

Chakula nyororo kama vile wali, uji viazi vilivyopondwa, uji wa maharagwe, mkate, samaki, matunda kama vile ndizi mbivu, machungwa, maembe na mananasi. Chakula cha mafuta si kizuri sana.

# **Kila mara endelea kumnyonyesha mtoto anayehara**

**Bi. Fatouma amefundishwa kuwa chakula kizuri kwa mtoto anayehara ni maziwa ya mama. Maziwa ya mama yanayeyuka haraka tumboni na yana nguvu ya kukinga mwili kutokana na viini.**

**Ni sharti watoto wanyonyeshwe pindi wanapotaka maziwa hata kama matokeo yake ni kuhara zaidi. Watoto wachanga sana ni rahisi kufa kutokana na ukosefu wa maji mwilini au njaa kwa sababu ya mazoezi mabaya wakati watoto wanapohara.**



**JINSI YA KUKINGA  
JAMAA YAKO KUTOKANA NA VIINI:  
Hifadhi maji ya kunywa ndani ya chombo  
kilicho na kifuniko**

**Je, kuna njia bora ya kuhifadhi maji?**

Haya maji ya kunywa yamehifadhiwa vyema kwa vile watoto hawawezi kuingiza mikono ndani wanapotaka maji ya kunywa. Mtungi una kifuniko na jerrycan pia ina kifuniko kwa hivyo, kuku na wanyama wengine hawawezi kuyachafua haya maji.

**Chombo cha aina gani ni kizuri kutumiwa?**

Manufaa ya kibuyu (jerrycan) ni kuwa mtu hawezi kuingiza mikono ndani lakini vigumu kuyamwaga haya maji wakati jerrycan imejaa na pia si rahisi kuisafisha.



Mtungi ni rahisi lakini lazima uwe na kata na ni lazima watoto wafundishwe vizuri kutoingiza mikono yao ndani ya maji.

# Nawa mikono kabla ya kutayarisha chakula

**Je, unaweza kuziona katika picha hii jinsi Hadija amezibadilisha njia zake za kupika?**

1. Sasa Hadija ananawa mikono yake kwa sabuni kabla hajagusa chakula.
2. Kiwanja cha nyumba yake ni safi hata hakuna nzi. Anafunga mlango ili nzi wasiingia jikoni ambako anatayarisha chakula chake.
3. Anawaweka mifugo nje na anahifadhi chakula kama kimefunikwa na hakiwezi kuchafuliwa.
4. Anawapa watoto wake vyakula aina zote tatu kwa vile anajua hiyo ndiyo njia bora ya kuzuia jamaa yake kutokana na magonjwa.



# **Kila mara nawa mikono na sabuni**

**Unaweza kuona jinsi jamaa ya Bi. Fatouma wanavyonawa mikono sasa?**

1. Sasa Bi. Fatouma anafahamu kuwa ni vibaya kwa kila mtu kunawa mikono kwa chombo kimoja katika maji yale yale tu.
2. Binti yake, Hadija, anamwagia maji mtoto wao mdogo anaponawa mikono.
3. Wote wananawa wakitumia sabuni.
4. Hawatumii taulo.

**Njia gani ambazo  
Fatouma anaweza  
kupata viini  
mikononi  
mwake?**



# Chakula salama ni chakula moto

Bi. Fatouma anajua kuwa chakula kikiachwa ovyo ovyo viini vitaingia ndani na kuharibika. Pia inzi watatua juu yake na kueneza viini. Chakula salama sana ni chakula moto kwa sababu joto huu viini.



## Aina gani ya vyakula vinaleta afya na vinafaa mwilini?

1. Chakula cha kujenga mwili: samaki, nyama, maharagwe, mayai, na maziwa.
2. Chakula cha kukinga mwili: mboga na matunda.
3. Chakula cha nguvu: mkate, ugali, viazi, wali na sukari.

# Safisha sahani pindi baada ya kula

Baada ya chakula Hadija anachukua vyombo vyote na kuviosha kwa sabuni punde tu baada ya kula. Anafahamu kuwa sahani chafu zinavutia inzi na inzi wanatawanya viini.

Sasa sahani zinawekwa juu ya meza ili zikauke na ziwe mbali na uchafu na wanyama ambao wanachafua kwa viini.



**Tumia mahali pa kukausha vyombo**





## **KICHOCHO**

**Kitu gani kinatendeka  
katika picha hii?**

Huyu mvulana amewaleta mbuzi mtoni kunywa maji. Mbuzi wanapokunywa maji kijana anaenda kujisaidia hapo karibu na mto. Kinyesi chake kitabebwa na maji ya mvua hadi mtoni. Ikiwa huyu kijana ana kichocho basi ataieneza kwa wale wote wanaotumia haya maji. Hiyo ndiyo njia mahsusi ambayo kichocho kinaenezwa.




Wakati mwingine watoto wanakojoa ndani ya maji. Hawa wavulana wana kichocho. Wakati mwingine wanaona damu katika kinyesi chao na mkojo pia huwa na damu. Damu hii inatoka kwa michango inayokaa ndani yao. Hii michango inataga mayai na yanatoka pamoja na kinyesi au mkojo. Mayai yanapoingia ndani ya maji yanaanguliwa na yanakuwa michango.

# Magonjwa tunayopata tunapooga kwa maji machafu

Watu wengi wanapata matatizo wanapooga au kutembea ndani ya maji machafu. Haya maji yanachafuliwa na viini vya wanyama na wanadamu.

## Magonjwa gani mengine tunaweza kupata kwa kuoga kwa maji machafu?

1. Kujikuna—hakuna alama ila unajikuna mwili mzima
2. Kidonda masikioni—maumivu ya masikio na usa kutoka
3. Pua kuzibika—mafua na pua kuzibika
4. Magonjwa ya macho—maumivu, macho mekundu na machozi kutiririka.
5. Kichocho.



# Dalili za Kichocho na jinsi ya kuiponya

## Nini inaweza kufanyika kwa watu wanaotembea au kuogelea ndani ya mto?


Mtu akiogelea au kutembea ndani ya mto au ndani ya matope kando ya mto, michango itatoboa ngozi yake na kuingia ndani. Punde michango ikiwa ndani itasafiri hadi kwenye tumbo. Hapa michango itakutana na baadaye kutaga mayai. Michango inapata chakula kutoka kwa huyu mtu, kwa hivyo, inamfanya kuwa mnyonge, ana maumivu ya tumbo na matokeo yake damu ndani ya mkojo na kinyesi.

## Je, kichocho kinaweza kutibiwa?

Watu wengi wanaoishi karibu na mto wana kichocho lakini hawajui kwa sababu wamezoea kuziona dalili hizi. Kichocho kinaweza kutibiwa katika zahanati (kliniki) iliyo karibu. Tatizo ni kuwa aliyetibiwa atapata kichocho tena pindi atakapoenda kwenye maji yaliyo na kichocho.

## Jinsi ya kutambua kama una kichocho?

1. Unachoka wakati wote
2. Una maumivu ya tumbo na mgongo
3. Damu kwenye mkojo na kinyesi.



Mayai kufika kwa maji katika wiki 3

Zinapaoagnliwa zinahitaji konokono katika masaa 18

Zinapotoka kwa konokono lazima zipati mtu kabla ya masaa 8

# Kuzuia Kichocho: No. 1

## Tunawezaje kuondoa kichocho?

Njia ya kuepuka kichocho ni kuharibu viini vyote vya kichocho majini. Hii itawezekana pindi watu wote watakaposhirikiana na kuhifadhi hali ya usafi. Hii ina maana kuwa watu wote watumie choo au wafunike kinyesi chao na wasijisaidie mtoni.

## Jukumu la umma ni nini?

1. Eneo la soko lazima liwe na vyoo vitakavyohifadhiwa na kamati ya kijiji. Wageni wasichafue mazingira kwa kujisaidia popote na matokeo yake ni kueneza kichocho kutoka sehemu zingine.
2. Kila mtu ahakikishe amefunika kinyesi chake akijisaidia mweituni.
3. Mashule yajenge vyoo na watoto wajifunze umuhimu wa kutumia vyoo kabla ya kuondoka shuleni kwenda nyumbani ili wasijisaidie njiani na kuchafua mazingira.





## **Usiwalishe chakula inzi. Kila mara chukua jembe**

Tabia nzuri sana Fatouma amefundisha jamaa yake ni kufukia kinyesi chao ama sivyo watakuwa wanalisha inzi na kueneza magonjwa katika jamii yote. Ye yote anayeenda kujisaidia mwituni lazima afukie kinyesi chake. Kwa njia hii wanasaidia kutekeleza wajibu wa afya bora. Kufunika kinyesi sio tu kunasaidia kupunguza kuhara lakini kunapunguza kuenea kwa kichocho.

Tabia za kizamani lazima ziachiliwe mbali kwani zinaenda kinyume cha bora afya.

# Kila mara nawa mikono baada ya kujisaidia mwituni

Hadija anajua umuhimu wa kunawa mikono baada ya kujisaidia kwa sababu anaweza kueneza magonjwa kama hatanawa mikono yake michafu.

Hana mtu wa kumsaidia anapotaka kunawa mikono yake lakini wametengeneza mahali ambapo anaweza kunawa bila msaada wowote.



## Mkebe unatoa maji.

Mkebe wowote unaweza kutumiwa. Toboa shimo dogo kwa upande wa chini wa mkebe na uutundike kwenye mti ullo karibu. Acha ndoo ya mayi hapa karibu ili iweze kujazwa kwa urahisi. Tengeneza kata ukitumia mkebe mwingine kwa kupigilia waya au kijiti ili uwe na mpini. Acha kipande cha sabuni hapa karibu ili mikono ioshwe vizuri. Jaza mkebe wenye shimo na maji na woshe mikono yako maji yanapotiririka kwa njia hii, maji mengi hataharibiwa.

# Kuzuia Kichocho No 2



**Lazima watu wote washirikiane ikiwa kichocho kinatakiwa kumalizika kabisa.**

1. Jenga bafu karibu na mtambo wa maji ya wanaume mbali, na ya wanawake na ya watoto kupunguza matumizi ya mto. Mijengo ya nyasi, na majani ya migomba ni rahisi kwa kununua pia ni rahisi kwa kujenga na kuhifadhi.
2. Sheria zinahitajika ambazo zitatenga sehemu za kuoga na kufua. Sehemu za kuchota maji na sehemu za mifugo kunywa maji.



# **Magonjwa tunayopata kwa kutooga vizuri**

Watu wengi wanapata magonjwa kwa vile hawaogi kila mara au hawatumi sabuni wanapooga ili kuondoa viini mwilini mwao.

## **Je, unajua magonjwa mengine ambayo hayajatajwa hapa?**

1. Impetigo—vidonda usoni hasa kuzunguka pua, masikio na kwenye matako.
2. Exema—vipele vyekundu mwilini hasa karibu na viungo.
3. Trachoma—ugonjwa ya macho unaolete upofu.
4. Vijidudu vinavyoishi juu ya mwili na vinaleta mwasho wakati wa usiku.
5. Chawa—vijidudu vinavyoishi ndani ya nywele kwa sababu ya uchafu.
6. Michango—michango huishi ndani ya miili yetu na hutumia nguvu yetu.
7. Majeraha na vidonda vinakuwa vibaya kama havitawekwa katika hali ya usafi.

**Kuzulia magonjwa haya oga kila siku kwa maji safi na sabuni. Ni muhimu sana kuziosha nyuso za watoto zikiwa chafu na hasa wanapokuwa na mafua. Kama sivyoy, basi uchafu utawavutia nzi ambao wataleta magonjwa kama vile ugonjwa wa macho na baadaye utaleta upofu.**

**Kuzulia kutawanyika kwa chawa na magonjwa ya ngozi, fua nguo zote na blanketi kila wiki.**




# **Kwa njia gani nyingine tunaweza kueneza viini kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine?**

1. Tukiwa na magonjwa kama mafua na flu na hali tunapumua kwenye watu, basi hawa watu wanapumua viini vya magonjwa.
2. Viini vinaenea wakati watu wawili wanapokutana kimwili k.m. Ukimwi.
3. Tukijikata viini vinaingia ndani ya damu zetu kutoka kwa chombo kilichotukata. (viini vya tetanus).

## **Tunawezaje kupunguza kutawanyika kwa viini kutoka mtu mmoja hadi mwingine.**

1. Tuhifadhi usafi ya mikono yetu kabla ya kugusa chakula.
2. Usipige chafya au kukohoa kwa kichwa cha mtu mwingine ukiwa na mafua. Usilale pamoja na watu wengine ukiwa mgonjwa.
3. Kutana kimwili na mtu mmoja tu ambaye unajua tabia zake. Tumia kibofu cha condom.
4. Safisha jeraha na vidonda na uviweke safi kwa kutumia vitamba safi.



# Magonjwa yanayohusika na maji

Magonjwa gani tunaweza kuyapata kwa kuishi  
karibu na maji?


Malaria na Malale ni maarufu sana. Ni vigumu kuyaondoa. Watu  
wameyazoea.



**KILA MARA KUNYWA MAJI KWA WINGI**

# Tunawezaje kupunguza malaria?

1. Tunaweza kutumia dawa kila wiki au kila siku ili kuzuia malaria.
2. Tunaweza kutumia vyandatumia na pia tunaweza kuweka nyavu za sengienge dirishani kuzuia mbu wakati wa usiku. Kunyunyiza au kuchoma dawa ya mbu hupunguza idadi ya mbu.
3. Hakikisha hakuna maji yanayosimama karibu na nyumba zetu kwa vile mbuu wanaangua mayai hapo.



## Je, Malaria huonywa viipi?

Unaweza kupata dawa ya Malaria kutoka hospitalini na ugonjwa atapona kwa haraka kama atatumia hizo dawa. Hata hivyo, jambo la muhimu ni kuona kuwa mgonjwa hakosi maji mwilini kwa kutokunywa maji. Maji masafi au kinywaji cho chote ni lazima kwa mgonjwa wakati wote kwa vile anapoteza maji mengi kwa kutoa jasho jingi.

# **Kama unajali afya ya jamii chungu maji**


Mtambo wa mkono unaweza kukaa kwa muda mrefu kama ikitunzwa na hii ni kazi ya watu wote. Ili kazi hii kufaulu chagua kundi la watu ambao wanatambua hili ni jukumu lao.

## **Ni akina nani wanotakiwa kwa kamati hii ya maji?**

1. Watu watano wachaguliwe kutoka kwa manyumba au kijiji ambacho kinatumia huu mtambo wa mkono.
2. Lazima wawe wanaheshimiwa, waaminifu na wanafahamu jukumu lao na hakuna uwezekano ya mmoja wao kuhama.
3. Kamati liwe mchanganyiko ya wanaume na wanawake.
4. Wachaguliwe kila mwaka.

## **Kazi yao ni nini?**

1. Wahakikishe mazingira ya mtambo inawekwa kwa hali ya usafi.
2. Wachimbe mfereji ili maji yanayomwagika yananyunyiza shamba la mboga ya umma. Ikiwezekana wajenge boma.
3. Lazima wajenge bafu la wanaume, wanawake na watoto karibu na mtambo ili watu wahifadhi siri zao.
